Nambari ya Mtahiniwa ___________________

SMZ

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA KUINGILIA KIDATO CHA KWANZA

125 URAIA

MUDA : SAA 2 : 00 JUMATATU 26 NOVEMBA, 2018 mchana

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu TATU (3) A, B na C.
2. Jibu maswali YOTE katika sehemu A na B. Chagua maswali MANNE (4) kutoka sehemu C.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu yote yaandikwe katika nafasi zilizowekwa.
5. Simu za mkononi haziruhusiwi ndani ya chumba cha mtihani.

| KWA MATUMIZI YA WASAHIHISHAJI | | |
|---|---|---|
| NAMBARI YA SWALI | ALAMA | SAINI |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| 7. | | |
| 8. | | |
| 9. | | |
| 10. | | |
| 11. | | |
| JUMLA | | |

Mtihani huu una kurasa 12 zenye maandishi

Nambari ya Mtahiniwa ____________________

SEHEMU A: (Alama 20)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii

1. Chagua jawabu sahihi kisha andika herufi yake kwenye jadweli liliyopo hapo chini.

i) Utaratibu wa uongozi unaoshirikisha wananchi katika maamuzi yanayohusu maisha yao

A. Utaifa B. Utandawazi

C. Demokrasia D. Utawala

ii) Moja kati ya zifuatazo si msingi wa kidemokrasia

A. Kujali na kuheshimu haki za binadamu

B. Kutoa na kupokea habari

C. Kushiriki katika mfumo wa vyama vingi

D. Kuwepo kwa demokrasia ya moja kwa moja

iii. Rangi ya kijani katika bendera ya Taifa humaanisha

A: Utajiri wa madini B. Raia wa Tanzania

C. Mimea D. Mito

iv. Kutokuwa na haraka ya kuhukumu, ni hatua ya

A. Utatuzi wa umasikini katika jamii

B. Utatuzi wa matatizo katika jamii

C. Kutii sheria za nchi

D. Kuepusha migongano katika jamii

v. Yafuatayo ni manufaa ya ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Madola isipokuwa

A. Kuuza mali ghafi inazozizalisha kwa nchi wanachama

B. Kupata misaada na mikopo kutoka nchi tajiri

C. Kushiriki katika michezo mbali mbali ya Jumuiya ya Madola

D. Baadhi ya nchi wanachama kujitoa katika jumuiya hiyo

vi. Makubaliano ya kuanzishwa kwa Umoja wa Afrika yalifanyika tarehe

A. 9/9/1999 B. 19/9/1989 C. 19/9/1979 D. 9/9/2009

vii. Watumishi wa umma wanatakiwa kuzingatia kipengele kimoja kati ya vipengele vifuatavyo

A. Usawa B. Maslahi C. Kanuni za kazi D. Ubunifu

viii. Chombo cha kimataifa kinacholinda na kuendeleza haki za binadamu

A: UNHCR B: UNO C: ILO D: IMF

ix) Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania huteuliwa na

A. Wabunge B. Spika wa bunge

C. Rais D. Katibu wa bunge

x) Mtu anapofanya kitendo cha uhalifu unatakiwa

A. Kumkamata mara moja B. Kutoa taarifa mahakamani

C. Kutoa taarifa sehemu husika D. Kuchukua sheria mikononi

JAWABU

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

2. Andika Kweli kama sentensi ni sahihi au Sikweli kama sentensi sio sahihi katika jadweli linalofuata.

i) Mmong'onyoko wa maadili ni moja kati ya athari za utandawazi.

ii) TAKUKURU ni taasisi ya kuzuia na kupambana na magendo.

iii) Mahakama ya wilaya kwa kawaida huwa inasikiliza kesi za jinai na madai ya fedha au mali.

iv) Rais wa Tanzania anapokuwa hayupo nchini nafasi yake hushikwa na Waziri Mkuu.

v) Sheria za msingi zinazotawala mwenendo wa siasa na serikali katika jamii huitwa Mahakama.

vi) Uwajibikaji ni sifa ya kiongozi bora.

vii) Moja ya kasoro za mfumo wa vyama vingi vya siasa ni kuchelewa kufikiwa kwa maamuzi.

viii) Lengo la Jumuiya ya Madola ni kuwepo kwa uhuru, usawa, haki na heshima ya binadamu.

ix) Ukosefu wa fedha si changamoto ya Umoja wa Afrika.

x) Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ilianzishwa mwaka 1977.

JAWABU

| i | ii | iii | iv | v | vi | vii | viii | ix | x |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | | | |

SEHEMU B: (Alama 40)

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii

3. Chagua majibu sahihi kutoka KIFUNGU B yanayoowana na maelezo ya KIFUNGU A.

| KIFUNGU A | KIFUNGU B |
|---|---|
| i) Upungufu wa kinga mwilini | A. 1977 |
| ii) Wajibu wa mwananchi | B. Mahakama |
| iii) Kuanzishwa kwa Umoja wa Mataifa | C. UKIMWI |
| iv) Idadi ya mikoa ya Zanzibar | D. Kulipa kodi na ushuru |
| v) Chombo cha serikali ya mkoa | E. 1945 |
| | F. Kipindupindu |
| | G. Mitano |
| | H. Kamati ya ulinzi na usalama |
| | I. Mitatu |
| | J. VVU |

JAWABU

| i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

4. Jaza mapengo katika sehemu zifuatazo.

i) Mifumo mikuu miwili (2) ya kisiasa ni ______________________________

na ____________________________________________________________

ii) Tabia zinazokubalika katika kundi la viongozi huitwa _________________

iii) Mahakama hupaswa kufanya kazi zake kwa uadilifu bila ya

_______________________________________________________________

iv) Ulinzi ni namna ya kujilinda dhidi ya ________________________________

v) Aina mbili (2) za rushwa ni _______________________________________

na ____________________________________________________________

5. Jibu maswali yafuatayo kwa ufupi.

a) i) Nini maana ya utandawazi?

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

ii) Andika nyanja mbili (2) za utandawazi.

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

_________________________________________________________

b) i) Ainisha faida mbili (2) za katiba isiyoandikwa.

______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________

ii) Onesha kasoro mbili (2) za katiba isiyoandikwa.

______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________

c) Toa tofauti moja (1) kati ya Serikali ya Wilaya na Serikali ya Mkoa.

______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________

d) Eleza kwa ufupi faida mbili (2) za ushiriki wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________
______________________________________________________________

e) Andika majukumu mawili (2) ya Mamlaka ya Kupambana na Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar.

SEHEMU C: (Alama 40)

Jibu maswali MANNE (4) tu katika sehemu hii

6. Elezea jinsi tunavyoweza kutatua matatizo ya umasikini na maradhi katika jamii.

7. a) Taja vikosi vitano (5) vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

b) Eleza kazi moja (1) ya kila kikosi ulichokitaja hapo juu.

8. Fafanua mafanikio manne (4) ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

9. Elezea kwa ufupi malengo manne (4) ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika.

10. Chambua matumizi matano (5) ya misaada inayopata Tanzania kutoka Umoja wa Afrika.

11. Chora mchoro elekezi wa muundo wa ngazi za mahakama katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.